

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA TURIANI (TURIANI WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-013-2018/2019

Mnamo tarehe 6 Septemba 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Turiani (Turiani WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake kwa kipindi cha 2018/19 - 2020/21. Majedwali namba 1-4 yanaonesha mchanganuo wa bei na ada za sasa zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Mabadiliko kwa asilimia	Bei Zinazopendekezwa				
	2017/18		2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	800	9%	870	4%	901	36%	1,225
Taasisi	845	9%	920	14%	1,046	24%	1,294
Biashara	945	9%	1,030	3%	1,056	37%	1,447
Viwanda	1050	9%	1,140	1%	1151.43	40%	1,608
Magati	20/ndoo ya lita 20	150%	50/ndoo ya lita 20	0%	50/ndoo ya lita 20	100%	100/ndoo ya lita 20

Jedwali 2: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Wateja Wasio na Dira – Shilingi/mwezi

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	3,600	54%	5,560	24%	6,890	30%	8,960
Taasisi	18,500	0%	18,500	11%	20,500	38%	28,200
Biashara	20,500	0%	20,500	39%	28,500	6%	30,100

Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuunganishiwa Huduma ya Majisafi - Shilingi/Maunganisho

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	20,000	NA	Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa vya Maunganisho ya Huduma ya Maji				
Taasisi	20,000	NA					
Biashara	20,000	NA					
Viwanda	-	NA					

Jedwali 4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Majisafi – Shilingi/Kurejeshewa Huduma

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000	25%	12,500
Taasisi	10,000	0%	10,000	25%	12,500	16%	14,500
Biashara	10,000	0%	10,000	35%	13,500	30%	17,500
Viwanda	-	NA	17,500	0%	17,500	14%	20,000

Sababu kuu zilizopelekea kuomba mabadiliko ya bei kama ilivyoenezwa na Turiani WSSA ni kumudu gharama za kukarabati na kubadilisha miundombinu, kuboresha huduma ya majisafi na kuongeza mtandao wa majisafi katika maeneo yasiyo na huduma ya Kunke, Msufini na Kijiji cha Lusanga A.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 6 Desemba 2018 katika Kituo cha Jamii kilichopo mjini Tuariani** kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali; Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA; wateja wa Turiani WSSA; na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 11 Desemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA MASHARIKI, GHOROFA YA SABA, JENGO LA LAPF; MKABALA NA JUMBA LA MAKUMBUSHO** au **MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ZILIZOPO MJI WA TURIANI**.

**Imetolewa na: Kaimu
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

8 Novemba 2018

